UWEKEZAJI

. . . kuwa na dakika hizi chache pamoja na nyinyi watu. Pia ninamshukuru Ndugu Pearry kwa ajili ya mwaliko huu wa kuwa hapa, na kwa ajili ya ushirikiano wenu wote.

2 Nafikiri hii ni ziara yetu ya tatu kwa mji wenu wa kupendeza. Daima tumeona watu hapa kuwa ni wema, na daima wanazungumza, tayari kusaidia, kama wanakujua, au sivyo. Nimezuru baadhi ya sehemu za biashara, na jinsi zinavyopendeza. Daima huonekana tofauti na jinsi ilivyo kule juu kaskazini penye baridi; wananiona nikiingia, wanakungoja na kuondoka, na ni hayo tu. Lakini ni nadra sana kutembelea mahali bila ya mtu kusema, "Asante! Rudi ukatuone tena!" Ninapenda hilo.

3 Basi, nafikiri kwamba Ndugu Pearry hapa, kwani ningemwita hivyo, ninii tu . . . Nina umri mkubwa kuliko baba yake, kwa hiyo nadhani ninaweza kumwita Ndugu Pearry. Kwa kweli hatukumjua mvulana huyo, isipokuwa alitambulishwa na mwanangu, Billy Paul, ambaye alienda shule pamoja na yeye. Lakini kama kuna mtu katika mji huu, ama karibu hapa, anayeweza kufikiwa na televisheni, ambaye atapotea katika siku ya mwisho, haitakuwa kwa sababu kwamba Ndugu Pearry hakuweka kila jitihada kujaribu kuwaleta watu kwa Kristo. Kwa kweli hakuacha jiwe hata moja bila kugeuzwa. Nami nayahesabu haya kuwa ni majaliwa makuu ya kuwa hapa.

4 Wakati Ndugu Pearry aliponiambia, ningeweza "kuzungumza kwenye dhifa ndogo" aliyokuwa nayo, kwamba baadhi ya wafanyabiashara wenzake wangekuwa hapa. Vema, mimi kwa kweli si mhubiri. Si—sidai kuwa hivyo, bali nilidhani ningeweza. Ingekuwa ni heshima kwangu, baada ya kuwa na mwaliko namna hiyo, kuwazungumzia wa—wa . . . wafanyabiashara wenzake.

5 Nina majaliwa ya kusafiri kimataifa, kote ulimwenguni. Na ninayahubiria sana Matawi ya Wafanyabiashara wa Full Gospel. Basi ninajua huu ni wakati mdogo tu wa ushirika, kwa hiyo ningependa kueleza jambo ambalo lilikuwa la kuvutia wakati mmoja. Kulikuwako na mtu, baada ya mimi kumaliza kuhubiri . . . Wote walikuwa ni wafanyabiashara. Na, kwa hiyo, pale nje palikuwa na jamaa aliyenijia, naye akasema, "Wewe ni mhubiri, sivyo?"

Nami nikasema, "Naam, bwana."

6 Akasema, "Kwa nini unaambatana na hawa wafanyabiashara?"

Nikasema, "Mimi ni mfanyabiashara."

Kwa hiyo akasema, "Loo, ndivyo ulivyo?"

Nami nikasema, "Naam, mimi—mimi ni mfanyabiashara."

Kasema, "Uko katika biashara gani, bwana?"

Nami nikasema, "Dhamana ya Uzima wa Milele."

7 Na yeye hakunielewa vizuri. Nililisema haraka. Alisema, "Loo, Bi—Bima ya Uzima wa Milele." Kamwe sikusema bima; nilisema dhamana, na yeye . . . Ila sikumwambia. Ndipo akasema, "Uzima wa Milele," kasema, "Sijui. Sidhani nimewahi kusikia habari zake hapo kabla."

Nikasema, "Hivyo ni vibaya sana."

Kasema, "Vema," akasema, "wapi makao makuu?"

Nikasema, "Mbinguni."

8 Ningali katika biashara hiyo. Ningependa kuzungumzia hati ya mkataba na yeyote wenu, baada ya ibada kumalizika, usiku wa leo. Nina shauku kubwa na kazi yangu. Basi, kwa hiyo, pia sikusema sasa, "bima," nilisema, "dhamana."

9 Bima ni sawa, mwelewe. Ninakumbuka . . . Kwa kweli, sina yoyote wakati huu.

10 Ninakumbuka, baada ya kuoa, mimi na mke wangu tulikuwa tumeketi nyumbani, siku moja. Basi rafiki yangu msiri . . . Ndugu yangu ni mwuza bima, Magharibi-Kusini. Mvulana huyu alikuwa ni mwuzaji wa Prudential. Nilienda shule pamoja naye, mvulana mzuri sana. Ndu—ndugu yake huandikia *Chumba Cha Juu*, kwani, ninaamini yeye ni mhudumu wa Kibaptisti, naye huandika makala katika maskini gazeti linaloitwa *Chumba Cha Juu*. Watu wazuri sana. Kwa hiyo alikuja kuniona, siku moja, ndipo akasema, akasema, "Billy, ni—ninasikia kwamba ulipata pigo wakati mmoja kwenye bima."

Nami nikasema, "Naam."

11 Akasema, "Kidogo ilikupa hisia kali kuwahusu?"

Nikasema, "Hapana, si hasa."

Akasema, "Niliwazia ningekuja na kujadili hati ya mkataba pamoja nawe, Billy."

12 Nami nikasema, "Vema," nikasema, "Wilmer, asante," nikasema, "bali ni—nina dhamana."

Naye akasema, "Loo, samahani."

13 Ndipo mke wangu akaniangalia, kana kwamba nilikuwa mnafiki. Alijua sikuwa na yoyote. Aliniangalia akiwa tu amestaajabu. Nikasema . . .

14 "Loo," akasema, "Samahani, Billy." Hapana shaka alifikiria nilikuwa nayo na kaka yangu, Jesse. Ndipo nikasema . . .

Mke wangu akaniangalia. Na yeye . . . Nikasema, "Naam, ninayo dhamana."

Ndipo akasema, "Uko na kampuni gani?"

Tena nikamwambia jambo lile lile, "Uzima wa Milele."

Naye akasema, "Loo," kasema, "hiyo ndiyo?"

15 Nami nikasema, "Naam. Nina: Dhamana iliyobarikiwa, Yesu ni wangu! Loo, ni kionjo cha jinsi gani cha utukufu wa Kiungu! Mimi ni mrithi wa wokovu, nimenunuliwa na Mungu, Nikazawa kwa Roho Wake, nikaoshwa katika Damu Yake.

16 Akasema, "Billy, hiyo ni nzuri sana. Ninathamini hiyo. Ila hiyo haitakuweka hapa juu kaburini."

17 "Lakini," nikasema, "itanitoa huko. Sina wasiwasi . . . " A-ha. Naam. Sina wasiwasi kuhusu kuingia; ni kutoka huko.

18 Bado ningependa kujadili na wewe hati ya mkataba, baada ya ibada, ikiwa . . . Nina hakika Hiyo ni sahihi.

19 Sasa, kwa kawaida mimi huwafanya watu wasimame tunaposoma Neno, lakini, usiku wa leo, nitajaribu kuacha hiyo kwa sababu ni vi—vigumu sana kwenu kusimama. Lakini kabla tu hatujasoma Neno, hebu tuinamishe tu vichwa vyetu kwa dakika chache, tunapozungumza na Mwandishi wa Neno. Kama vile tumekuwa tukibishana sisi kwa sisi, na kwa namna fulani kuachilia, ama, kama tusemavyo, "kujiachilia baada ya kubanwabanwa." Kwa hiyo hebu tuende upande wa kicho sasa, na uaminifu, na kuigeuza mioyo yetu kuelekea Mbinguni tunapolifungua Neno. Sasa mtu yeyote awezaye kusogeza mikono yake anaweza kuifungua Biblia, bali hakuna mmoja ambaye anaweza kwa kweli kufungua ufahamu ila Roho Mtakatifu mkuu, kwa hiyo hebu tuzungumze na Yeye.

20 Baba yetu wa Mbinguni, hakika tumefurahia, usiku wa leo, kukutanika hapa na kundi hili la watu, upande huu wa Umilele, na kuwa na ushirika huu wa kupendeza. Basi tunapoketi kuzunguka meza hizi, usiku wa leo, tukitazamana mmoja na mwenzake upande mwingine, na wafanyabiashara wenza na—na Wakristo, tunajua kwamba kunakuja wakati mwingine ambapo tutakutana. Tunaamini kwamba sote tutakuwa Huko, kila mtu akiwepo kwenye karamu kuu ya Arusi huko hewani, wakati Mfalme atakapojitokeza, ayapanguse machozi yote kutoka machoni petu, na kusema, "Ni vyema, watumishi Wangu wema na waaminifu, ingieni katika raha za Bwana, mlizoandaliwa tangu msingi wa ulimwengu."

21 Iwapo kuna wengine, Bwana, ambao hawakujui Wewe katika njia hiyo, nami ninaomba usiku wa leo kwamba jambo fulani litafanywa au kusemwa litakalowasababisha kuibadili njia ya mawazo yao, wakugeukie Wewe; iwe ni waliopo hapa, ama kupitia nji—njia ya televisheni, ama kupitia kanda ambazo zitasambazwa kutokana na huu.

22 Tubariki pamoja sasa, na ubariki kusomwa kwa Neno Lako. Igeuze mioyo yetu na mawazo kuelekea mwisho wa maisha

haya, na kile kitakachokuwa hali yetu wakati huo. Kwa kuwa tuna hakika, Baba, kwamba sote hatuna budi kuondoka kwenye ulimwengu huu. Sisi ni wanadamu wapatikanao na mauti, basi jalia tumtazamie Yule wa Milele, Yule wa pekee awezaye kutupatia Uzima baada ya haya. Kupitia Jina la Mwana Wake, Yesu Kristo, tunaomba hayo. Amina.

23 Ningependa kuita usikivu wenu, kwa dakika chache sasa, kwenye kusomwa kwa Neno la Mungu. Ningependa kuanza kusoma kutoka kwa Injili ya Marko Mtakatifu, nafikiri mlango wa 10, na kuanzia kifungu cha 17.

> *Hata alipokuwa akitoka kwenda njiani, mtu mmoja* akaja *mbio,* akampigia magoti . . . akamwuliza, akisema*, Mwalimu mwema, nifanye nini nipate kuurithi uzima wa milele?*
>
> . . . *Yesu akamwambia, "Kwa nini kuniita mwema? Hakuna aliye mwema ila mmoja, ndiye Mungu.*
>
> *Wazijua amri, Usizini, Usiue, Usiibe, Usishuhudie uongo, Usidanganye, Waheshimu baba yako na mama yako.*
>
> *Akajibu akamwambia, Mwalimu, haya yote nimeyashika* tangu *utoto wangu.*
>
> *Yesu akamkazia macho, akampenda, akamwambia, Umepungukiwa na neno moja. Enenda, ukauze ulivyo navyo vyote, uwape maskini, nawe utakuwa na* hazina *mbinguni; kisha njoo ukabebe msalaba* wako*, unifuate.*
>
> *Walakini yeye akakunja uso kwa neno hilo, akaenda zake kwa huzuni; kwa sababu alikuwa na mali nyingi.*

24 Bwana na aongeze baraka Zake kwa Neno tunapodhamiria kutoa kwenye hili fungu na muktadha. Sasa nikiwazia somo la kuwa na wafanyabiashara, na daima ninafikiria kwamba wafanyabiashara daima wanavutiwa na—na uwekezaji mzuri, ili kwamba niliite somo sasa kwa dakika chache zijazo: *Uwekezaji*.

25 Mfanyabiashara mzuri siku zote anatafuta u—uwekezaji mzuri, imara. Kama sivyo, basi yeye si mfanyabiashara mzuri. Hana budi kutafuta kitu kilicho halisi.

26 Nami ningependa kuwazungumzieni juu ya mwaliko niliowapa dakika chache zilizopita, juu ya hati hii ya mkataba wa Uzima wa Milele, kama nilivyojitambulisha mwenyewe kama m—mfanyabiashara. Basi ninayo biashara, na ningependa kuwazungumzieni kwa dakika chache juu yake. Na Maandiko machache nimeandika hapa, na fungu, ningependa kutumia haya kwa dakika chache, muhtasari huu.

27 Si bi—biashara nzuri kubahatisha. Mtu yeyote anajua hilo, kwamba bahati nasibu si biashara nzuri, kwa sababu ni kubahatisha. Kamwe, au ni nadra kumwona mtu anayebahatisha . . . Siku moja yeye ni tajiri, na kesho yake

anaombaomba. Kwa hiyo unajihatarisha sana, ku—kubahatisha. Nafikiri m—m—mwenye kubahatisha kwa—kwa kweli anaishi tu mara moja, wala haangalii mbele katika siku za usoni, la sivyo asingekuwa akibahatisha.

28 Na, vile vile, siamini katika baadhi ya huu uwekezaji wa kutajirika ghafla, kwa biashara fulani isiyotambulikana. Sasa, mfanyabiashara yeyote mzuri asingejihatarisha namna hiyo, labda kwa ha—hazina yako ya maisha, mapato yako; na ungeyawekeza katika kitu fulani cha kuja karibu, kutajirika upesi mno. Na hakijatambulikana. Mtu fulani anakuja mbio na namna fulani ya wazo, kwamba, "Hapa tu—tuna kampuni fulani hapa," haijulikani inakotoka. Nafikiri mtu mzuri, mwenye akili timamu angekuwa mjinga kuwekeza katika ka—kampuni kama hiyo.

29 Kwa sababu, nilikuwa na rafiki, wakati mmoja, ambaye—ambaye alijaribu kitu kama hicho. Na, alipofanya hivyo, a—alipoteza kila kitu alichokuwa nacho, na akapoteza mapato ya maisha yake yote. Akiwa karibu kustaafu, na aliwazia, "Vema, nita—nitajaribu bahati hii," kwa sababu mtu huyo ilionekana kuwa alijua alichokuwa anazungumzia. Bali, akaja kugundua, ka—kampuni hiyo ilikuwa tu ni kampuni ya kujifanya, na hakuna bidhaa wala chochote, kwa hiyo maskini jamaa huyo alipoteza kila kitu alichokuwa nacho.

30 Kwa hiyo nafikiri, mtu akitaka kufanya uwekezaji mzuri, kwanza anapaswa kuichunguza kampuni yake, ama chochote kile anachowekezea, na ajue kile anachoenda kufanya. Nafikiri mtu yeyote mwenye akili angefanya hivyo.

31 Halafu basi tena, kabla sijaendelea, ningependa kusema, si wazo jema kuweka pesa zako katika mfuko wako. Watu wengi wanasema, "Nita—nitaziweka tu mfukoni mwangu, na ni—ni . . . na ninazo." Lakini, mnajua, nyinyi wanaume na wanawake wafanyabiashara, hamwazii kwa njia hiyo. Na si jambo jema, kwa sababu zinaweza kuibiwa.

32 Ni vizuri zaidi kuziweka katika matumizi. Kama vile Bwana alisema, wakati mmoja, Yeye alitoa karama nyingi sana kwa wengi sana, na hivyo, na kisha yeye . . . walizitumia katika uwekezaji. Na wale waliofanya uwekezaji mzuri, thabiti, Yeye aliwapa faida. Lakini wakati mtu yule mmoja aliposema, "Ni—niliiweka tu. Si—sikutaka kubahatisha nayo. Ni—ni—niliiweka mfukoni mwangu. Ama, niliizika mahali fulani." Ndipo Yeye alichukua kile alichokuwa amempa, na kumpa yule aliyekuwa amepata faida nyingi, aliyeiweka katika kitega uchumi kizuri. Na hiyo ndiyo njia ya Bwana wetu ya kufanya mambo.

33 Sasa, bali kama ulikuwa unaenda kuwekeza katika kitu ulichotaka kuwa na hakika nacho, ungetafuta kampuni fulani nzuri, ya kutegemewa ambayo imethibitishwa kwamba itakunufaisha vizuri. Sasa, huo ni uwekezaji mzuri, thabiti.

Baada ya kuijaribu kampuni hiyo, unajua historia yake, umezungumza na mtu ambaye amefanya biashara na kampuni hii, na kusikia ushuhuda wa kila mtu, "Ni asilimia mia moja. Kila mara wanatoa mgao wao wa faida kwa wakati ufaao. Pia—pia kuna rasilimali nyingi nyuma yake, hata kampuni hiyo haifilisiki." Basi huo ni uwekezaji mzuri, thabiti. Tena sasa, kote katika maisha, watu wamefundishwa hayo.

34 Sasa tunazungumza usiku wa leo juu ya Maandiko, kuhusu mvulana mdogo wa Kiebrania, ambaye alikuwa ki—kijana aliye tajiri. Huenda alitoka kwenye nyumba nzuri kwelikweli, hapana shaka. Ushuhuda wake ulionyesha kwamba alikuwa ametoka kwenye nyu—nyumba nzuri. Aliitwa, katika Biblia, "mtawala kijana tajiri." Ninaenda kuibadilisha usiku wa leo, kidogo tu, niseme, "mfanyabiashara kijana tajiri," kwa sababu alikuwa na biashara, naye alivutiwa na—na biashara. Na hapana shaka baba yake alikuwa mfanyabiashara mashuhuri aliyefanikiwa, ama labda asingalikuwa na kile alichokuwa nacho. Lakini alikuzwa kuwa—kuwa mfanyabiashara.

35 Naye aliona kitu fulani ndani ya Jamaa huyu kijana wa Galilaya, Nabii huyu kijana Jina lake Yesu wa Nazareti. Hapana shaka alishamsikia kuhani wake akinena habari Zake, na labda dhidi Yake. Lakini alipopata kumtazama kwa mara ya kwanza Bwana Yesu, kulikuwa na kitu fulani kumhusu Yeye kilichokuwa tofauti na mtu yeyote mwingine.

36 Nami nasema hili, kama Mkristo, kwa kweli haijabadilika. Tuna wanatheolojia mashuhuri nchini, kote ulimwenguni, tumekuwa nao kwa maelfu ya miaka, ambao wanaweza kutuanzishia ka—kanuni ya imani. Nao wamefunzwa katika kanuni hizo za imani, na kanisa ambalo—ambalo ni kanisa lililoimarishwa vizuri. Lakini hiyo ingali siyo ha—hati yangu usiku wa leo ninayozungumzia. Ninazungumza kuhusu Uzima wa Milele.

37 Basi jamaa huyu kijana, akijua kwamba alikuwa ni mshiriki wa kanisa, bali aliona ndani ya Yesu kitu tofauti. Kwa hiyo alipewa fursa ya kuwekeza, wakati alipompata Yesu na kuona yale aliyokuwa akifanya. Na alikuwa ameisoma Biblia yake, na kuona ndani ya Yesu kwamba kitu kile ambacho amesikia manabii wake wakisoma katika kanisa lake, na kile walichokuwa. Na hapana shaka alikuwa amesoma hiyo. Ndipo basi wakati alipoona katika huyu Yesu wa Nazareti, ambaye alidhaniwa miongoni mwa watu, kuwa Nabii, aliona kitu fulani katika Mtu huyu kilichomtambulisha Yeye na Maandiko.

38 Nami nafikiri, leo hii, haijabadilika sana. Wasomaji wa Biblia na wapenzi wa Biblia, wakati hasa tukipata mtazamo katika akili zetu, wa kile Yesu alichokuwa na kile alicho, hubadilisha msimamo wetu wote. Hakuna yeyote kama Yeye, haijalishi alivyo mwema. Tulisema tunaelewa kwamba Yeye . . .

Tunadhani Yeye hakuwa na elimu nyingi, na Yeye alizungumza kama mtu wa kawaida, na kuvalia kama mtu wa kawaida, na kuishi na watu wa kawaida. Lakini hata hivyo kulikuwa na kitu cha kipekee kumhusu Mtu huyu, na hicho kilivutia usikivu wa jamaa huyu kijana. Kwa jinsi, hata, alikuwa na mali yote ya ulimwenguni, labda, ambayo alihitaji na angetumia katika maisha yake, na alitosheka kabisa na hiyo. Lakini aliona kwamba Mtu huyu aliangalia siku za usoni na kuwaambia mambo yaliyokuwa yanakuja, na kujitambulisha Mwenyewe katika Maandiko, na Mungu akajitambulisha Mwenyewe katika Mtu huyo.

39 Sasa hakuna mtu aishiye, aliye na akili timamu, ila ambaye daima hushangaa alikotoka, yeye ni nani, na anaenda wapi? Kumekuwako na vitabu vingi vimeandikwa, wanafalsafa wameinuka na kuanguka. Bali kuna Kitabu kimoja tu kitakachokuambia kuwa wewe ni nani, mahali ulikotoka, na mahali unakoenda, na hicho ni Biblia. Hicho ndicho Kitabu pekee. Kati ya vitabu vyote vizuri tulivyo navyo, ungeweza kuvipuuzia, kila kimoja. Hii ndiyo Kweli. Chochote kinyume na Hii si sahihi. "Mbingu na nchi zitapita, bali Neno Langu halitashindwa kamwe. Neno la kila mtu litakuwa uongo; la Mungu litakuwa kweli."

40 Basi wakati ukiona kitu dhahiri sana mbele zako, na Maandiko yaliyoahidiwa kwa ajili ya siku hiyo, kile Masihi huyo alipaswa kuwa. Ndipo huyu kijana aliona hicho kimetambulishwa na Mungu, basi hiyo ilimfanya Yesu kuwa tofauti kabisa na mtu mwingine yeyote aliyekuwa amemwona. Kwa hiyo, alipewa fursa.

41 Alipompata Bwana Yesu, na labda kumwona katika mikutano Yake na ibada Yake, alimkimbilia na kuanguka miguuni Pake, ikionyesha kwamba nia yake ya kumwendea ilikuwa sahihi.

42 Ndipo akasema, "Mwalimu Mwema, ningeweza kufanya nini ili kuwa na Uzima wa Milele?" Sasa hilo ndilo jambo linaloulizwa. Si pesa zake, au la, "Je! ningeweza kujiunga na kanisa Lako, Bwana? Ama je! ningeweza kujiunga na shirika Lako?" Bali, "Nifanye nini ili niwe na Uzima wa Milele?" Hilo lilikuwa ndilo swali.

43 Basi alipewa fursa ya kupokea Hilo, bali alifanya uamuzi wa kijinga. Alikuwa . . . aliikataa. Hakuvutiwa, wakati alipopata kujua kile kilichohusiana nalo. Alitambua, kwamba ili kufanya jambo hili, ilimbidi kuacha umaarufu wake. Kwa sababu, Yesu hakuwa maarufu, hakuaminiwa miongoni mwao, ningesema bila kufikiri, asilimia tisini ya watu, ama labda ilikuwa asilimia tisini na tano. Hakuaminiwa, kama "mtu fulani mwenye roho chafu," na aliitwa, na wengi, "Beelzebuli," shetani.

44 Na, hata hivyo, Maandiko yakimtambulisha kikamilifu. Alikuwa amerejea hayo, akisema, "Yachunguzeni Maandiko, kwa kuwa ndani Yake mnadhani mna Uzima wa Milele. Na Hayo ndiyo Hayo yanayonishuhudia Mimi, ama kuwaambia kuwa mimi ni Nani."

45 Mvulana huyu wa Kiebrania, akiwa amelelewa nyumbani, na akijua kwamba Biblia ilikuwa—ilikuwa imewaambia wazi, vyuo. Mungu Yehova alikuwa amesema kwamba, "Akitokea mtu miongoni mwenu, aliye wa kiroho, ama nabii, Mimi Bwana nitajitambulisha Mwenyewe kwake katika maono. Na ikiwa yale asemayo yanakuja kutimia, basi msikieni nabii huyo, kwa kuwa niko pamoja naye. Lakini yasipotimia, basi msiyasikie hayo."

46 Hiyo ni lugha wazi. Ni mawazo ya busara tu. Kama alisema hilo, nalo halitendeki, basi ni uongo; Mungu hakulisema. Lakini akisema, nalo li—linatendeka, hilo ni kweli; na hakuna lililo kweli zaidi, zaidi ya kweli.

47 Kwa hiyo jamaa huyu kijana alikuwa ameona haya katika Bwana Yesu, na akajua kwamba Yeye alikuwa na funguo za huu Uzima wa Milele, naye alitaka Uzima huu wa Milele, ila aliikataa fursa yake ya kuwekeza. Hakuvutiwa na uwekezaji wa namna hiyo. Ingawa ninii . . .

48 Alitambulishwa vizuri kwamba Yeye alikuwa ni Mwana wa Mungu. Ametambulishwa kikamilifu. Bikira alikuwa amechukua mimba, akamzaa Mwana. Alikuwa amefanya kila ishara ambayo Masihi alipaswa kufanya.

49 Lakini ili kumkubali Yeye, ilimbidi kuondokea mapokeo yake. Ilimbidi kuyaacha.

50 Tungependa kuchanga hilo tu kwa ninii . . . mvulana huyu wa Kiyahudi, lakini ni vibaya sana inatubidi pia kutambua hilo, leo hii, vivyo hivyo. Ni gharama kubwa. Tunaweza kuchangia makanisa ya leo. Na mara nyingi, watu wanaojiita waaminio, huku hawako tayari kujitenga wenyewe na kuyaondokea mambo ya ulimwengu, kama mtawala huyu kijana alivyoulizwa afanye, ili kuwa na hati ya Uzima wa Milele. Hata hivyo, baadaye, sisi pia tunaliona Hilo likitambulishwa vizuri na Maandiko, kwamba Hati za mkataba zingali zinatolewa kwa yeyote atakaye kupokea Hiyo.

51 Kama nilivyosema, aliona kitu fulani ndani ya Yesu, hakuna mtu alikuwa nacho, bali gharama ilikuwa kubwa mno hata hakutaka kulipa gharama.

52 Ni jambo lile lile leo hii. Kama ninavyoamini, usiku wa leo, huenda ninazungumzia madhehebu mbalimbali, Methodisti, Baptisti, Presbiteri, Katoliki ya Rumi, Orthodoksi ya Kiyahudi, Budha, chochote kingine, hao ndio wafanyabiashara wa mijini. Lakini kunayo, kweli, ukiona jambo fulani kwa macho yako mwenyewe, ambalo Maandiko yanatambulisha kuwa kweli; tungekuwa watu wasio na akili kabisa, kwamba, ikiwa

tunatamani Uzima wa Milele, kulikataa Hilo. Ungekuwa ni u—uamuzi wa kijinga kama huyu kijana alivyofanya. Mara nyingi, hata maaskofu wetu leo hufanya kosa lili hili la kijinga, ingawa ni wasomi hodari katika kanuni za imani, wanaozijua vizuri. Lakini, kumbuka, wale makuhani katika siku ile walijua vyuo, vizuri sana, pia, bali walikosa kuona kile kijana huyu alichoona.

53 Naye alivutiwa na—na Yesu kumpa Uzima wa Milele. Bali alipojua ulichokuwa unaenda kumgharimu, basi hakupendezwa.

54 Mnajua, Biblia inatwambia, katika wakati huu tunaoishi. Kama vile Ndugu yetu Pearry hapa mwenye fadhili ametufafanulia, kwamba aliamini kwamba ilikuwa katika siku za mwisho. Kwa hakika, kabisa ninaamini hilo kwa moyo wangu wote. Ninaamini Maandiko yanatambulisha hilo.

55 Ninaamini kwamba—kwamba—kwamba sayansi inatambulisha hilo. Wanasayansi wanasema, "Ni dakika tatu ifike usiku wa manane." Ninii—ninii . . . Vipindi vyetu tunavyoona kwenye televisheni na—na kwenye redio, na—na jinsi watu wetu wanavyotenda, ni . . .

56 Kama nilivyotoa tamshi hapa au mahali pengine, kwamba inanikumbusha, kwa hayo yasiyofaa yote wanayofanya, inanikumbusha juu ya mvulana mdogo anayepitia makaburini wakati wa usiku, akipiga mbinja, akijaribu kujifanya afikirie kwamba si mwoga, bali ni mwoga.

57 Hiyo ndiyo shida ya kugeuka kwetu kwa yote tufanyayo leo hii, ya matendo yetu maarufu yasiyofaa. Tunajaribu kuwafanya watu wafikirie kwamba hatujui kwamba wakati umekaribia, bali tunajua umekaribia. Wanasayansi wetu wanajua hilo. Nanii wetu . . . Pentagon inajua. Sote, sisi sote tunajua kwamba kuna jambo linalokaribia kutendeka. Wewe, wewe unaweza kulihisi moja kwa moja angani, nasi tunajua limekaribia.

58 Nayo Biblia yetu inatuambia, katika Ufunuo mlango wa 3, kwamba kanisa katika wakati huu litatambulishwa kama vile tu mvulana huyu wa Kiebrania, tajiri, kijana, "tajiri, hawana haja ya chochote," wakati huu wa Laodikia. Iwapo kuna wahudumu hapa, ama wasomaji wa Biblia. Huu ndio wakati wa Laodikia. Pia ilisema, "Kwa kuwa mimi ni tajiri, limeketi kama malkia, halina haja ya chochote." Kasema, "Hivi hujui kwamba wewe u mnyonge, maskini, kipofu, mwenye mashaka, uchi, nawe hujui." Jambo la kuhuzunisha la nukuu hii ya Maandiko ni . . .

59 Kama tulimwona mwanamume ama mtu mtaani, aliyekuwa ni kipofu na uchi na mwenye mashaka na maskini, hilo lingekuwa ni ta—tamasha la kuchukiza. Hakuna mmoja ila wote wangewakimbilia upesi wawezavyo, na kusema, "Rafiki, uko uchi. Huna budi—huna budi . . . Uko uchi hadharani. Njoo uingie ndani, upesi, na—na—na hebu nikupe nguo. Halafu nitakupeleka mahali fulani kuona kama ninaweza kumpata tabibu, ili waweze

kukurejeshea kuona kwako," ama kujaribu kumfanyia jambo mtu huyo.

60 Vipi kama ulikutana na mtu kama huyo, nao wangekugeukia na kukuambia ushike lako? Hata hawajui wako katika hali hiyo. Sasa iwapo uko hivyo, na unajua, si vibaya sana. Lakini ukiwa hivyo, nawe hujui, hiyo ndiyo sehemu mbaya. Huwezi kuwaambia.

61 Nalo Andiko hili halina budi kutimia, kama vile Maandiko yote hayana budi kutimia. Biblia ilisema kwamba hii ingekuwa ndiyo hali katika siku za mwisho. Pia wamemkataa Yesu, na Yeye alikuwa nje ya kanisa, akijaribu kuingia ndani. Wamelikataa, hadharani tu kama kijana huyu wa Kiyahudi alivyofanya. Na hili lilikuwa ni kanisa la Mataifa, kanisa la Bibi-arusi, lililoitwa litoke, linaloitwa "kanisa la Kikristo" katika siku za mwisho, bali walimtoa nje kwa sababu ile ile kijana huyu mfanyabiashara wa Kiyahudi aliyomtupia nje. Gharama ilikuwa kubwa sana. Wasingaliweza kulipokea Hilo.

62 Biblia ilisema hapa kwamba walikuwa "tajiri," ikasema "hawakuwa na haja ya kitu." Mvulana huyu mdogo alikuwa tajiri, hakuwa na haja ya kitu. "Sisi ni dhehebu zuri ambalo limejenga utaratibu mkuu. Tunao udugu. Tuna yote *haya*, *yale*, au *mengineyo*. Tumekuwa na kanuni zetu za imani kwa hayo mamia ya miaka. Tumeweka. Hatuna haja ya kitu. Usituambie chochote kuhusu Hilo!"

63 Vema, huo ni mtazamo wa kijeuri zaidi ya ule aliochukua kijana huyu. Hakuchukua mtazamo kama huo. Biblia ilisema, kwamba, "Yesu alimtazama akampenda."

64 Sijui leo hii, ikiwa miongoni mwa mchafuko wetu wote na kupenda kwetu mambo ya ulimwengu, na hata hivyo tunajaribu kushikilia maungamo yetu ya Ukristo, kama si upendo wa Mungu unaoshurutisha huduma kuendelea. Nashangaa kama si kitu kile kile, kama hapa tunamkuta Yeye akibisha mlangoni, akijaribu kuingia ndani. Sasa tunaona mambo haya, yote katika nyakati, imekuwa hivi.

65 Sasa, ili kuokoa wakati, kuizungumzia hati ya mkataba tena, na kwa muda kidogo tu kuwafafanulia.

66 Sasa mvulana huyu tajiri, yeye hakuomba kujiunga na kanisa Lake. A—alikuwa mshiriki wa kanisa. Ilithibitisha hiyo.

67 Yesu alimwambia, "Zitii amri. Wewe wazijua. Usizini. Usiibe. Usiseme uongo, kudanganya. Na—na ufanye, pia—pia waheshimu baba na mama yako."

68 Ndipo jamaa huyu kijana alithibitisha kwamba alikuwa ni m—mvulana mwema, aliyestaarabika, si kile tu ambacho tungekiita leo hii, ja—jambazi. Alikuwa ni mvulana mwema, aliyelelewa katika nyumba nzuri. Akasema, "Mwalimu, nimetenda haya tangu nilipokuwa mvulana, maisha yangu yote."

Unaona, ilionyesha kwamba wazazi wake walikuwa ni wazazi wazuri. Alihudhuria kanisa lililoamini kutii amri. Lakini hata hivyo, kuwa kanisani, kutii amri, bado hakukujibu lile aliloona ndani ya Yesu. Alijua.

69 Pamoja na kanuni yetu ya imani na pamoja na kanisa letu, na kuzitii amri, bado hazitupi Uzima wa Milele. Hazikufanya wakati ule, wala hazifanyi leo. Kuna jambo linalokubidi kufanya.

70 Sasa, tunaona kwamba haikuwa ati kwa sababu hakuwa mshiriki wa kanisa. Haikuwa kwa sababu hakuwa mzuri kimaadili. Alikuwa.

71 Lakini tunaweza kuwa mshiriki wa kanisa, na mwenye maadili mema, bado hatujapokea Uzima wa Milele. Si kulijua Neno; baadhi yao ni wanatheolojia, na wasomi, na walimu wa shule ya Jumapili, wafafanuzi wa Biblia, bali hayo hayamaanishi chochote. Shetani anaijua Biblia hiyo vizuri kuliko yeyote wetu. Biblia ilisema, "Kumjua Yeye ni Uzima," si kulijua Neno. "Kumjua Yeye ni Uzima." Shetani pia anaamini na kutetemeka. Bali inatubidi kupata tukio la kufa, kuzikwa, na kufufuka, kutoka kwa maisha yetu ya kale, hadi kwa Maisha mapya ambayo huja ndani ya Kristo. Huja tu kwa Roho Mtakatifu, Maisha mapya.

72 Sasa hebu tuwachunguze baadhi ya watu hawa kote kupitia nyakati, waliokuwa na hati hii ya mkataba, na tuone kama ina faida au la. Ndipo basi ningetaka tu kuwaletea, kama nilivyowaambia mwanzoni, kwamba unapaswa kutaka mtu ushauri unapoenda kuwekeza; tafuta kujua kile ambacho hufanyika, ni kitu gani, kama inalipa vizuri. Unapaswa kufanya hivyo katika biashara yako. Ninataka kuwazungumzia baadhi ya wale walioshikilia hati hii ya mkataba.

73 Ninavuta usikivu wenu, usiku wa leo, nyuma katika Mwanzo, kwa nabii jina lake Nuhu. Ingawa alijaribiwa kwa kila njia aliyoweza kujaribiwa, kwa kila njia Shetani aliyoweza kumjaribu, kumfanya aachilie hati hiyo ya mkataba; lakini Nuhu alishikilia ahadi ya Mungu, hati ya mkataba wa Uzima, maana Mungu alimwambia kwamba kila kitu nje ya safina hiyo kingeangamizwa, na ingawa lilionekana kwa namna fulani lisilo la kawaida kwa watu wenye mawazo ya kisasa katika siku yake.

74 Hiyo ndiyo inayofanya Injili leo hii. Ni kule kutokuwa kawaida, kwa sababu Mungu ni asiye wa kawaida. Neno Lake linatafsiriwa visivyo kawaida kwa kile ambacho sisi wakati mwingine hutafsiri Hilo.

75 Lakini, kama nilivyosema awali, Mungu hamhitaji mtu yeyote kulifasiri Neno Lake. Yeye hujitafsiria Mwenyewe kwa—kwa kufanya kutimia yale mambo aliyosema Yeye angefanya. Yeye hulitafsiri Neno Lake Mwenyewe. Hahitaji tafsiri yetu. Ni,

tafsiri yetu ni mawazo yetu wenyewe ya kujibunia ya mawazo ya wanadamu tunayoingiza katika Hilo.

76 Wakati Mungu aliposema, “Iwe nuru,” na kukawa nuru. Hilo halihitaji tafsiri yoyote.

77 Mungu alisema, “Bikira atachukua mimba,” naye akachukua. Hilo halihitaji tafsiri yoyote.

78 Yesu alisema, “Mwana wa Adamu anapanda kwenda Yerusalemu na kutiwa mikononi mwa watu wenye dhambi. Watamsulubisha, na kwenye siku ya tatu atafufuka tena.” Hilo halihitaji tafsiri yoyote.

79 Alisema, “Kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena; bali ninyi mtaniona, kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hadi mwisho wa wakati, hadi ukamilifu.” Yeye yupo hapa. Halihitaji tafsiri yoyote. Ni ahadi Yake.

80 “Kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya. Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo yeye naye atazifanya.” Hilo linapatikana katika Yohana Mtakatifu 14:12. Na sisi tunajua kuwa hilo ni kweli, kwa hiyo halihitaji tafsiri yoyote.

81 Nuhu, akiwa na Neno la Mungu, alishikilia Hilo, kwa sababu alikuwa mmiliki wa hati ya mkataba wa bima ya Maisha, dhamana ya Maisha. Alikuwa na hati ya mkataba. Na yeye alikuwa ni wakala kwa ajili ya hati hiyo, naye alienda kila mahali. Lakini kwa sababu haikupendwa na watu, asingeweza kupata mtu yeyote kuichukua, familia yake tu. Alikuwa . . . Ha—hati yake ilionekana kuwa iliyopitwa na wakati kabisa, kwa watu. Ilionekana kuwa kinyume cha mawazo ya kisayansi ya siku hiyo. “Mvua kushuka chini kutoka mbinguni.”

82 Haikuwa imewahi kunyesha juu ya nchi, kumbukeni. Ulimwengu ulisimama wima. Tunaweza kuthibitisha hilo leo hii, kwamba ulisimama hivyo wakati mmoja. Na Mungu alitilia mimea maji kupitia umwagiliaji, kutoka kwenye chemichemi ndani ya ardhi.

83 Sasa sayansi, katika siku hiyo, labda walikuwa werevu kuliko walivyo sasa, kwa sababu walijenga masfinksi na piramidi, na—na kadhalika, mambo ambayo tusingeweza kujaribu kufanya leo hii. Hatuna nguvu zinazoweza—zinazoweza kufanya hayo, lakini walivijenga. Nami ninadhani labda walipiga picha mwezi kwa rada ama chochote walichokuwa nacho katika siku hiyo.

84 Yesu alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu,” ustaarabu mwingine unaofananishwa na huo, “ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwa Mwana wa Adamu.”

85 Tunaona hapa hivi majuzi ambapo walichimba mfumo wa kisasa wa ugavi wa maji hapa katika Meksiko ya kale, hatuna historia yake, hata kidogo. Mnaona, huenda ilitoka katika wakati fulani mwingine uliopita.

86 Yesu alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku hiyo,” watu werevu, wenye akili. Lakini kama ilikuwa, basi kutakuwa na hati ya mkataba wa Uzima itakayotolewa kwa watu. Alisema hivyo.

87 Basi, Nuhu, huenda asiweze kueleza. Kama sayansi ilivyosema, “Tunaweza kuchukua vyombo na kuthibitisha hakuna mvua huko juu. Bwana, umerukwa na akili.” Lakini bado alijua ile Sauti iliyonena naye ilikuwa ni Mungu.

88 Kwa hiyo kama Mungu alikuwa amesema, “Kulikuwa kunakuja maji kutoka juu,” ingawa hakukuwa na maji, Mungu ni Elohimu, Yule aishiye peke yake. Ni Yeye anayejitosheleza. Kama Yeye alisema, “Kunaweza kuwa na maji huko juu,” Yeye anaweza kuweka maji huko juu, kutimiza Neno Lake.

89 Baba yetu Ibrahimu, ambaye katika baba wa mataifa mengi. Kama kulitokea kuwa na watu Wayahudi wameketi karibu, wanashangaa vile Mataifa walivyoingizwa ndani, Ibrahimu alikuwa ni baba wa mataifa mengi. “Naye hakuyumbayumba katika ahadi ya Mungu kwa kutokuamini.” Alishikilia hati ya mkataba pia. Mungu alikuwa amempa ahadi, kuwa baba wa mataifa mengi; siyo tu mataifa ya Kiebrania, bali mataifa mengine, ambayo angekuwa baba yao.

90 Tazama, kama alivyofanya, ahadi ambayo Mungu alimpa ilikuwa ya kijinga, katili. Alikuwa na umri wa miaka sabini na tano, naye Sara alikuwa na sitini na tano, kabla hajapata ahadi. Bali alijitenga mwenyewe kutoka kwa wasioamini, kwa sababu alijua alikuwa ndiye mrithi wa haki kwa mapenzi ya Mungu, na haijalishi ilichukua muda gani!

91 Labda mwezi wa kwanza ulipita naye akamwambia Sara, “Unajisikiaje?”

“Hakuna tofauti.”

92 Kasema, “Tutampata mtoto huyo, hata hivyo. Mungu alisema hivyo. Endelea na utengeneze vijibuti. Weka kila kitu tayari. Mungu alisema tutampata. Hilo latosha.”

Mwaka wa kwanza ukapita. “Mpenzi, unajisikiaje?”

“Hakuna tofauti.”

93 “Vema, itakuwa ni mwujiza mkubwa zaidi kuliko ilivyokuwa kama ingetendeka mwezi wa kwanza.”

94 Unaona, alikuwa yapata miaka kumi baada ya kukoma hedhi wakati ahadi ilipotolewa. Hawakuwa na watoto. Mke alikuwa ni tasa, naye mume alikuwa mgumba. Kwa hiyo wao . . . Lakini angali aliishikilia hati hiyo ya mkataba, kwa sababu ilikuwa ni Neno la Mungu, ahadi. Hakuwa anaenda kuachana nayo. Nayo Biblia ilisema, kwamba, “Ibrahimu hakusita katika ahadi ya Mungu kwa kutokuamini; bali alikuwa na nguvu, akimsifu Mungu; akijua hili, kwamba, Yeye anaweza kufanya kile alichoahidi kufanya.” Kwa hiyo mtoto huyo alizaliwa, kwa sababu kwamba alishikilia ha—hati ya mkataba.

95 Nuhu alishikilia hati yake ya mkataba, nayo ikaokoa maisha yake. Hiyo ilikuwa ndiyo faida. Siyo tu maisha yake, bali maisha ya familia yake; ililipa, kwa kuwaokoa.

96 Hebu tuzungumze na mwekezaji mwingine katika bima hii ya Uzima wa Milele. Danieli nabii, wakati ambapo vile tungeweza kusema . . . Kama mtasamehe hilo, kama tamshi la kilimwengu; sipaswi kulitoa, nadhani, hapa kwenye mimbara. Ndiyo njia ya pekee nijuayo kuieleza, "mambo yakiwa magumu sana." Mfalme Nebkadreza alikuwa amekuja na kuwachukua wana wa Israeli kwa sababu walikuwa wamemwacha Mungu. Walikuwa; wangali wakifanya matambiko yao yote.

97 Wakati Mungu alipowataka kutoa wana-kondoo na mafahali, na kadhalika. Mwanamume, Myahudi mwema, aliteremka barabarani, akiwa na fahali aliyenona au—au—au maskini mwana-kondoo chini ya mkono wake. Kwenye siku ya upatanisho, alishuka kwenda kumtoa kwa ajili ya dhambi yake. Alikuwa mnyofu wakati alipomwua mwana-kondoo huyo, ndipo kuhani akamchinja. Naye aliweka mikono yake juu yake, akijua kwamba uhai uliondolewa kuokoa uhai wake. Alikuwa mnyofu katika hilo. Na mradi tu alikuwa mnyofu, ilikuwa sawa. Lakini wakati uliwadia ambapo ilifanyika desturi ya jamii. Ndipo Mungu akasema, Yeye alimtuma nabii jukwaani, jina lake Isaya, Yeye akasema, "Sadaka zenu, sikukuu za makini, zinanuka katika pua Yangu."

98 Hapo ndipo sisi watu tumefikia. Tumejiunga na kanisa. Ambalo, ni sawa, tunafanya mambo hayo. Lakini, unasema, je! wewe ni Mkristo? "Mimi ni Mmethodisti. Mimi ni Mbaptisti. Mimi ni Mpresbiteri, Pentekoste, ama kitu kingine." Ni desturi. Hakuna kuingia, katika unyofu, tena. Hawatasonga, wakubaliane na Maandiko na kadhalika. Wanaishi tu kwa njia yoyote watakayo. Wakipata mchungaji anayejaribu kuwarekebisha, wanamtupa nje. Hawana uhusiano wowote naye ikiwa hawezi kuleta Hollywood kanisani; karamu, karamu za karata, milo ya supu, na kila kitu kingine; kuwaacha wanawake watende kwa njia yoyote watakayo, na kuvalia vyovyote watakavyo, kizinifu, chochote kile. Kuvutia kizinifu kunakuwa m—mtindo wa kisasa. Ni aibu.

99 Yesu alisema, kwa yule mwanamke. Unaweza kuwa mwadilifu uwezavyo, bali utawajibikia uzinzi kwenye siku ya hukumu, wewe unayevaa nguo hizo. Yesu alisema, "Yeyote amtazamaye mwanamke, kwa kumtamani, amekwisha kuzini naye tayari moyoni mwake." Basi haijalishi jinsi usivyo na hatia, huyo mwenye dhambi atawajibikia uzinzi, na wewe ndiye uliyeleta huo. Enyi Wakristo, hamna aibu? Mnapaswa kutenda kama binti za Mungu.

100 Nanyi wanaume, washiriki wa kanisa, mashemasi, hata kwa wahudumu, mtakaoowaruhusu wake zenu kufanya hayo,

mnapaswa kuwa wana wa Mungu. Hiyo haisikiki kama tabia ya mwana wa Mungu mwenye asili ya Baba yake ndani yake. Unaogopa kusema jambo kwa sababu dhehebu lingeweza kukufukuza. Hiyo ni kweli.

101 Danieli alikusudia moyoni mwake kwamba hakuwa anaenda kuichafua rasilimali yake. Alikusudia, "Haijalishi kile ulimwengu, jinsi mfalme anavyotajirika, na ni kiasi gani anavyojaribu kuniingiza katika mambo ya ulimwengu, sitafanya hivyo. Sitachafua rasilimali yangu."

102 Ee ulimwengu wa Kikristo, usichafue rasilimali yako uliyowekeza katika Uzima wa Milele. Utaichafua.

103 Danieli alikusudia kwamba asingefanya hivyo. Ikamnufaisha, kwa kuokoa maisha yake wakati alipotupwa katika tundu la simba. Rasilimali yake ililipa kabisa.

104 Wana wa Kiebrania walidhamiria kwamba hawangesujudia sanamu. Na ililipa, kwa kuokoa maisha yao katika tanuri la moto.

105 Ndipo akaja Simoni Petro, Farisayo mzuri aliyekuwa amefunzwa na baba yake, kwamba siku itakuja ambapo—ambapo atakuja Masihi. Kote kupitia nyakati, watu Wayahudi walikuwa wameitazamia. Na hapana shaka kwamba baba yake alikuwa amemwambia, "Mwanangu . . . " Ni—nilisoma hadithi ndogo wakati mmoja, kuhusu hilo, huenda ilikuwa ni ya kubuni. Sisemi kwamba ilikuwa ya kweli.

106 Bali alisema, "Nimeutazamia wakati wa kuja kwa Masihi." Pia kasema, "Ni—ni—ninajua kwamba kabla wakati huo kuja, kutakuwa na kila namna ya itikadi, mambo ya uongo yakiendelea. Ila, mwanangu, kama Mwebrania, tumefundishwa, kama Waebrania, kuwaamini manabii wetu, kwani Neno la Bwana huwajia manabii, na huyo pekee. Bwana alisema, 'Sifanyi lolote isipokuwa ninawafunulia manabii Wangu kwanza.' Naye huyu Masihi, kulingana na Musa, 'Bwana Mungu wako atamwinua nabii miongoni mwenu, kati ya ndugu zenu, aliye kama mimi.' Naye Masihi hatakuwa mwelimishaji. Hatakuwa dhehebu. Atakuwa nabii, na Neno la Bwana litakuwa pamoja Naye."

Andrea alikuwa amemsikia Yohana akizungumzia kuja kwa mmoja kama huyo, "yule Mbatizaji."

107 Lakini basi, siku moja, Simoni mwenyewe alitembea akaingia katika Uwepo wa huyu Yesu wa Nazareti. Basi punde tu Yeye alipomwona, alisema, "Jina lako ni Simoni, nawe ni mwana wa Yona." Alitoa hati ya mkataba upesi sana. Alijua huyo alikuwa ndiye Masihi. Huyo alikuwa ni Maandiko yaliyothibitishwa ya siku yake, Masihi. Wengine walikosaje kuona hilo?

108 Kulikuwako mmoja amesimama, jina lake Filipo, aliyeenda yapata maili kumi na tano kuzunguka mlima, kwa jamaa aitwaye Nathanaeli. Walikuwa wamekuwa na masomo ya Biblia pamoja. Labda maongezi yao yalikuwa kitu kama hiki, alivyompata chini ya mti, akiomba. Akasema, "Nathanaeli." Bila shaka, akiwa ni mtu mwuungwana aliyemfuata Yesu; mtu yeyote anayemfuata Yesu atakuwa mwuungwana. Kwa hiyo alimpata akiomba; a—akangojea kidogo. Lakini unaona, hakuzungumza naye kuhusu vijisitu vyake vya mzeituni ama kadhalika. Alienda moja kwa moja kwenye alama, "Njoo, mwone Yule tuliyempata: Yesu wa Nazareti, mwana wa Yusufu."

Kasema, "Sasa, laweza kuwepo lolote jema kutoka Nazareti?"

Akasema, "Njoo, uone."

109 Hilo ndilo jibu zuri kuliko yote mtu yeyote angaliweza kumpa mwingine. "Njoo, ujionee mwenyewe. Usikae nyumbani na kukosoa. Njoo, uichunguze mwenyewe."

110 Njiani wakizunguka, maongezi yao huenda yalikuwa namna hii. Labda Nathanaeli alisema, "Unajua, tumekuwa tukimtazamia Masihi, kwa miaka. Unajua, Filipo, jinsi ambavyo tumechunguza hili. Mbona, ninaamini Masihi ajapo, Mungu atavuta ushoroba Mbinguni na kufanya ushoroba mkuu kushuka, ngazi moja kwa moja juu ya (yetu) uwanja mkubwa wa hekalu alipo Kayafa kuhani wetu mkuu, ndipo Yeye atasema, 'Nipo hapa.'" Unaona? Bali hivyo sivyo jinsi Maandiko yalivyosema Yeye angekuja.

111 Yeye atakuja tu jinsi Maandiko yalivyosema. Alipaswa kuja katika nabii kama vile tu Musa alivyokuwa, mtu wa kawaida, mchunga kondoo.

112 Tazama, basi alipokuja katika Uwepo wa Masihi, na Yeye alikuwa kwenye mstari au akiwaombea wagonjwa, ama chochote kile alichokuwa anafanya. Tunaona kwamba Masihi anamwangalia, na akasema, "Tazama Mwisraeli ambaye hamna hila ndani yake."

113 Sasa huenda ukafikiria ilikuwa ni kwa sababu alivalia namna hiyo. Lakini, kumbuka, watu wote wa Mashariki walivalia sawa, kilemba na ndevu, kadhalika. Kumbukeni, Yesu alitembea pamoja nao, pia, barabarani kuenda Emau, siku nzima, baada ya kufufuka Kwake, na wao hata hawakumjua. Alivalia kwa namna ile ile.

114 Kwa hiyo tunaona kwamba katika Uwepo huu Wake mkubwa, alisema, "Rabi." Kijana huyu mzuri wa Kiebrania alisema, "Rabi, Wewe ulinijua lini? Wewe ulipata kunijua lini, kunijua kuwa ni M—Mwisraeli, na mwaminifu, sifa niliyo nayo? Hujawahi kuniona hapo kabla. Ulipataje kunijua?"

115 Ndipo Yeye akasema, “Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya mti, nilikuona.”

116 Alitoa hati ya mkataba. Akaangukia miguuni Pake kama alivyofanya kijana huyu mwingine, kasema, “Rabi, wewe ni Mwana wa Mungu. Wewe ndiwe Mfalme wa Israeli.” Jina lake linadumu leo hii.

117 Kuna maskini mwanamke, huenda nikamzungumzia kwa sababu ya kina mama wanaosimama karibu. Maskini mama huyu hakuwa kama nyinyi. Alikuwa na la—lawama ya uadilifu dhidi yake, na kanisa. Labda mtoto fulani mdogo alikuwa ametolewa akaenda huko nje mtaani, kimakosa. Labda wazazi wake hawakuwa wamemtunza. Alikuwa nusu Myahudi na Mmataifa; alikuwa ni Msamaria.

118 Kumbuka, kuna jamii tatu pekee za watu, kama Maandiko yetu ni sahihi.

119 Na Mungu anisamehe kwa hata kutaja “kama” Hayo ni sahihi. Ni sahihi. Hayo ni Mungu Mwenyewe. “Hapo mwanzo kulikuwako Neno, nalo Neno lilikuwa pamoja na Mungu, na Neno lilikuwa Mungu. Nalo Neno likafanyika mwili likakaa miongoni.” “Yeye yule jana, leo, na hata milele.”

Kwa hiyo msichana huyu mdogo alitolewa nje.

120 Kwanza, huenda nikaeleza watu wa Ham, Shem na Yafethi. Sasa sisi, Mataifa, tulikuwa makafiri katika siku hizo, tulikuwa tunaabudu sanamu, lakini Myahudi na Mtaifa walikuwa wakitazamia Masihi. Na Yeye huwajia wale tu wanaomtazamia.

121 Wakati mwingine leo hii, tunasema tunamtazamia Yeye, na kuweka mamilioni na mabilioni ya dola katika vitu, na kujenga taasisi na kadhalika. Nashangaa. Huku wamishenari wakifa njaa hudumani, ninawajua, huko nje usiku wa leo wakihubiri, bila jozi ya viatu mguuni. Tunaweka mamilioni na mamilioni ya dola katika upuuzi, na halafu, mbona, matendo yetu wenyewe yanahukumu ushuhuda wetu.

122 Lakini hapa msichana huyu, tunavyomfahamu, alikuwa ni Msamaria. Yesu alikuwa njiani Mwake akienda Yeriko, ambao uko chini ya Yerusalemu. Lakini Yeye alizunguka kupitia Samaria na akafikia mji unaoitwa Sikari, ndipo akatuma wanafunzi wake kununua maakuli, vyakula. Basi walipokuwa wameenda, msichana huyu akaja kuteka maji, ndipo Yeye—Yeye akamwambia, “Nipe maji ninywe.”

123 Naye akaangalia kote, akamwona Yeye akiwa ni Myahudi, akasema, “Si jambo la kawaida kwamba Wewe uniombe hayo.” Kasema, “Wewe ni Myahudi.”

124 Akasema, “Lakini kama ulijua ni Nani ulikuwa unazungumza naye, ungeniomba Mimi maji. Nikupe maji usije hapa kuchota.”

125 Basi mazungumzo yakaendelea, kuhusu dini, hatimaye Yeye akawasiliana na maisha ya mwanamke huyo. Akasema, "Nenda kamwite mumeo mje hapa."

Mwanamke akasema, "Sina mume."

126 Kasema, "Umesema kweli. Umekuwa na watano, na yule unayeishi naye sasa si mume wako."

127 Sasa siku chache kabla ya hapo, waalimu na marabi wa siku hiyo, watu waliopaswa kujua vema zaidi, walisema, "Yeye ni Beelzebuli. Anafanya hayo kwa roho mwovu." Iliwapasa kujibu kusanyiko lao. Kwa hiyo waliunda, wakasema, "Ni roho mwovu."

128 Ndipo Yesu akasema, "Nitawasamehe kwa hilo," upatanisho haukuwa umefanywa. "Bali atakapokuja Roho Mtakatifu kufanya jambo lilo hilo, kunena dhidi Yake hakutasamehewa," na sisi tunajua lilifanyika wakati Tito, baada ya wao kumkataa Roho Mtakatifu, Tito aliteketeza hekalu na kuwatawanya Wayahudi kuenda kote ulimwenguni. Na ndio sasa wanakusanyika tena, inatimiza Maandiko.

Sasa, tazama, sasa huyu mwanamke kijana.

129 Wakati, wale Wayahudi walipoona hilo likifanywa, na kumwita Huyo, "roho mwovu, roho mchafu," Biblia ilisema, "kumwita Roho wa Mungu, akifanya kazi, Roho mchafu, ibilisi," kama vile mpiga ramli ama mtu fulani mwovu.

130 Ndipo basi, upesi, mwanamke huyu alijua tofauti. Wakati Yeye aliposema, "Nenda kamwite mumeo."

Mwanamke akasema, "Sina mume."

131 Akasema, "Umesema kweli, maana una watano, na yule unayeishi naye, si mume wako."

132 Tazama hili. Upesi alisema, "Bwana, naona ya kwamba Wewe ni nabii." Kumbuka, hawakuwa wamekuwa na manabii kwa karibu miaka mia tano. Malaki alikuwa ndiye nabii wa mwisho wa Kiebrania. "Sisi, sisi tunajua kwamba Masihi yuaja, na huu utakuwa ndio utambulisho wa Masihi. Tunajua, wakati ajapo Yeye, hili ndilo atakalofanya."

Yesu akasema, "Mimi Ndiye ninayezungumza na wewe."

133 Naye akachukua hati ya mkataba. A-ha. Naye akaingia mjini, kutangaza Habari njema, kwamba alikuwa amempata Masihi. Alikuwa na Uzima wa Milele kwa sababu alikuwa amemwamini Yeye. Alijuaje? Aliona utambulisho wa Maandiko ukidhihirishwa na Yeye.

134 "Tunajua kwamba, wakati Masihi akija. Miaka mia nne hatujawa na nabii, na, wakati ajapo Yeye, huyo atakuwa ndiye mtu atakayefuata jukwaani. Sasa wakati ajapo, tutamjua Yeye, na Yeye anapaswa kufanya jambo lile lile."

135 Kasema, "Mimi Ndiye." Akachukua hati ya mkataba. Alivutiwa nayo.

136 Nikodemo. Dakika chache, katika kufunga sasa. Nikodemo, rabi, mtu wa yapata umri wa miaka themanini. Alikuwa ameshawishika kwamba kulikuwa na jambo kumhusu Yesu ambalo lilikuwa tofauti na watu wengine, kwa hiyo alitaka hati ya mkataba. Kwa hiyo akaja usiku, kwa ajili ya hiyo hati, naye akaikuta benki ikiwa wazi kwa ajili ya biashara. A-ha.

137 Daima imefunguliwa. Imefunguliwa kwenye dhifa. Imefunguliwa huko nje mtaani. Imefunguliwa mahali popote palipo na mtu yeyote aliye tayari kufanya biashara, hati hii ya mkataba na yule anayeishikilia.

Aliikuta benki ikiwa wazi. Akachukua hati ya mkataba.

138 Sasa tunajua, katika Luka 24:49, baada ya Yesu kuwachagua wanafunzi Wake, walikuwa ni wamiliki wa hati ya Uzima wa Milele. Kwa hiyo sasa, mnajua, katika hati ya bima ya kawaida, daima wanalipa mgao wa faida. Kwa hiyo walikuwa tayari wamekubalika na kuchaguliwa na Yesu, kwa hiyo wakaenda huko Yerusalemu, wakingojea hadi Siku ya Pentekoste, kupata mgao wao wa faida. Na ililipa, na ubatizo wa Roho Mtakatifu, na uweza wa kumdhihirisha Yesu Kristo.

139 Methodisti, Baptisti, Presbiteri, Othodoksi, yeyote yule uliye, mnaodai kuwa ni Wakristo, kwa nini msifanye vivyo hivyo? Unaamini Yesu Kristo na kuwa mshiriki wa kanisa, kwa nini usiendelee hadi Pentekoste, upokee mgao wako wa faida, nguvu za Roho Mtakatifu! Hao wenye hati ya mkataba waliupokea. Unaweza, pia, ikiwa unaiamini na kuiamini kweli.

140 Petro akiwazungumzia, alisema, "Ahadi ni kwa ajili yenu na watoto wenu, kwa walio mbali, wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu." Walitaka kujua jambo la kufanya. Akasema, "Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu." Ilikuwa ni ahadi.

141 Kwa hiyo kama wewe unakiri tu, usiku wa leo, wala hujapokea mgao wako wa faida, mbona usiilete hati yako, usiku wa leo, hebu niijadili na wewe kwa muda mfupi. Piga magoti pamoja nami kwa dakika chache na uone kama sivyo ilivyo. Kuwa mwaminifu kuhusu hiyo. Itatoa faida sasa hivi, kama kweli unashikilia hati. Yeye ataitambua hati hiyo, imani yako, kama unasema kuwa ni katika Mungu. Ikiwa ni katika Mungu na katika Neno Lake, na si katika kanisa fulani ama kanuni ya imani ya kidhehebu, ila tu ni kumwamini Yesu Kristo, itatoa faida. Yeye anaijua hati Yake Mwenyewe.

142 Nikimleta mhusika mwingine, kwa dakika chache tu. Kulikuwa na Mwebrania mwingine tajiri aliyekutana na Yesu siku moja baada ya kifo Chake, kuzikwa, na kufufuka.

143 Iwapo kuna Mwebrania hapa, usiku wa leo, ama yeyote yule uliye, Yeye kusulubishwa si kisingizio chochote ila kwamba unaweza kukutana na Yeye papa hapa, sawa tu na vile—vile tajiri mtawala kijana alivyokutana na Yeye. Kama unataka hati ya mkataba, Yeye yupo hapa kufanya biashara.

144 Kulikuwa na mtu jina lake Sauli, naye alifunzwa katika mafunzo yote makuu na mapokeo ya watu wake. Gamalieli alikuwa ndiye mwalimu wake, mmoja wa walimu wazuri sana wa Kiebrania wa wakati huo. Naye Sauli alikuwa na juhudi sana za hili, hata akampiga mawe Stefano, ama kushuhudia Stefano, ama kuidhinisha hilo. Alishikilia makoti ya wale, huku akiidhinisha, akiwa na mamlaka kutoka kwa kuhani mkuu kuwatupa watu hao wote, wa hati hiyo, gerezani, kwa sababu alikuwa ameambiwa na wazee wake, kwamba, "Mtu huyu hakuwa nabii. Mtu huyu hakuwa chochote ila ni mwenye siasa kali." Naye alikuwa na nyaraka mfukoni mwake, akishuka kwenda, kwa sababu alisikia kulikuwa na wengine huko chini Dameski, waliokuwa na hati hiyo ya mkataba. Nao walikuwa wamepata faida juu yake, nao walikuwa wanafanya mambo kwelikweli.

145 Basi kuhani mkuu alimwambia, "Sauli, wewe ni mtu mwenye bidii. Chukua mamlaka haya, kutoka kwangu, nenda huko chini na umtie mbaroni kila mmoja wao, kwa sababu wao si kitu ila wenye siasa kali, hawana chochote. Shuka uende ukawafunge, na kuwatupa gerezani. Ikikubidi kuwaua, waue, ni sawa. Nenda ukawashike!"

146 Sauli akasema, "Mheshimiwa, bwana, baba mtakatifu, nitaenda." Akashuka akaenda.

147 Akiwa njiani kwenda, alikuwa anaenda yapata saa tano mchana, akikaribia mji huo. Ghafla, kutoka mbinguni kukaja Nguzo ya Moto, ikamwangusha chini. Basi akainuka kuangalia, na hapo kulikuwa ile Nguzo ya Moto mbele zake.

148 Sasa ili kuwathibitishia hilo. Yeye alikuwa ni Mwebrania, na asingeweza kusujudia chochote ama kuita chochote Bwana, isipokuwa awe alijua kilikuwa ni Bwana. Naye alijua, kama mwalimu chini ya Gamalieli, kwamba Malaika wa Bwana, ambaye alikuwa ni Logos iliyotoka kwa Mungu, ambayo ilikuwa ni Kristo aliyewaongoza kupitia nyikani, alikuwa katika umbo la Nuru, Nguzo ya Moto. Basi wakati Hiyo ilipomwangusha chini, naye akaangalia juu na kuona Hiyo pale, alisema, "Bwana." Sasa, asingeweza kamwe kuita chochote ila Hiyo, Bwana. Lakini, akiwa ni Mwebrania, alijua kwamba Hiyo ilikuwa ni Yehova. Hiyo ndiyo sababu alikuwa na ufunuo, angeweza kusema kwamba Yesu wa Agano Jipya alikuwa ni Yehova wa la Kale. Huo ulikuwa ufunuo wake, maana alikuwa amemwona Yehova. Ndipo akasema, "Bwana, U Nani Wewe?"

149 Akasema, "Mimi ni Yesu, na ni vigumu kwako kuipiga teke michokoo." Ndipo akaitoa hati ya mkataba.

150 Walinganishe watu hao wawili pamoja. Mwebrania mmoja tajiri aliyetaka kushikilia mapokeo yao; mwingine aliyeshawishika. Mmoja wao alimwona Yeye kama mwanadamu, kwamba Mungu alifanyika mwili ili aweze kufa na kuondolea mbali dhambi.

151 Damu ya wana-kondoo na kadhalika, uhai uliokuwa mle, usingeweza kuja juu ya mwaminio, kwa sababu ni uhai wa mwana-kondoo, hauna nafsi ndani yake, uhai wa mnyama. Bali huyu alikuwa ni Mungu Mwenyewe, na, ndipo tunazaliwa kwa Roho huyo, sisi ni wana na binti za Mungu, Uhai uliokuwa juu ya Kafara yetu.

Walinganishe watu hao wawili pamoja.

152 Akaona Hiyo imethibitishwa, kwamba Mungu alikuwa ndani ya Kristo. Nguzo ile ile ya Moto iliyokuwa imewaleta watu Wake kupitia nyikani, na kuwaleta mpaka pale, ikawatunza siku nzima. Kumbuka, wakati Yesu alipokuwa duniani, Yeye alisema, "Nimetoka kwa Mungu, na ninaenda kwa Mungu." Alikuwa ndiye ile Nguzo ya Moto iliyowaongoza watoto kupitia nyikani.

153 Biblia ilisema, ya kwamba, "Musa aliuhesabu utajiri wa Kristo kuwa ni hazina kuu kuliko ule wa Misri." Aliiacha Misri, kumfuata Kristo.

154 Wakati Yeye alipokuwa hapa, hiyo Nguzo ya Moto iliwakilishwa katika Yeye, Mungu. Alisema, "Kama sizifanyi kazi za Baba Yangu, basi msiniamini Mimi. Kazi zinawaambieni yale ninayopaswa kufanya. Nisipofanya hayo, basi msiamini. Lakini ikiwa hamwezi kuniamini Mimi . . . "

Wakasema, "Wewe ni—Wewe ni mwanadamu unayejifanya Mwenyewe Mungu."

155 Kasema, "Ikiwa hamwezi kuniamini Mimi, kama Mtu, amininі kazi. Zinanishuhudia Mimi." Mnaona?

156 Sasa, wakati Yeye alipokufa, akazikwa, akafufuka, akapaa, hapa tunampata tena katika ile Nguzo ya Moto. Alikuwa ametoka kwa Mungu, na akaenda kwa Mungu.

157 Angali ni Yeye yule, Yeye yule sasa. Tazama, hakika, Yeye yule aliyekuwa.

158 Ndipo wakati Paulo, ama Sauli wakati huo, alipotambua kwamba Mungu Yehova, ile Nguzo ya Moto ya Agano la Kale, alikuwa amejiita Mwenyewe Yesu, alitoa hati yake ya mkataba. Alikuwa tayari kwake wakati huo.

159 Ni uamuzi wa kijinga jinsi gani kwa yule mtawala kijana! Ni ninii . . . Jinsi ambavyo hapana shaka alininii . . . Nini, angeifanyaje? [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

160 Ungetoa nini kubadilisha na nafsi yako? Baada ya majengo yako yote, na u—unayaacha kwa jamaa zako kuzozania, na kila kitu, vipi kuhusu nafsi hiyo na mahali unakoenda kuwa? Kumbuka, utakuwa mahali fulani, maelfu ya miaka kuanzia usiku wa leo. Huenda huu ukawa ni wakati wako wa kufanya uamuzi wako.

161 Tazama ni kosa la kijinga jinsi gani huyu mfanya-. . . Ni m—ni mfanyabiashara wa jinsi gani aliyekuwa, kujaribu kushikilia kwenye mapokeo, wakati ilikuwa imehakikishwa kwake na kuthibitishwa kwamba Hapa palikuwepo Uzima wa Milele, na yeye akashuhudia hivyo kwa kumwuliza Yesu habari zake.

162 Paulo aliikubali. Tunajua jinsi alivyotoka. Kama vile watu wa siku hizi, wanapenda mawazo maarufu, na sifa za wanadamu badala ya heshima ya Mungu. Paulo hakujali sifa za wanadamu. Aliitaka heshima ya Mungu.

163 Hebu tumfuate mvulana huyu mdogo kwa muda mfupi tu kabla hatujafunga. Hebu tumfuate. Tunapata mahali pengine, ambapo, jamaa huyu mdogo, mnajua kilichofanyika kwake? Hakufanyika maskini, kwa kufanya hili. Hakufanyika ombaomba barabarani. Mali yake iliongezeka. Alikuwa ameikataa fursa.

164 Mara nyingi, watu leo hii watacheka na kudhihaki Roho Mtakatifu, halafu waendelee na kupanuka katika biashara yao. Mnajua, samahani tamshi hili . . . Lakini wakati wanapocheka, waseme, "Mbona, angalia, mimi! Kama kuna lolote kwa Hilo, unaona, mbona, lingetendeka kwangu, jambo fulani lingetendeka kwangu."

165 Mnajua, kuna me—me—methali, kwamba, "Wapumbavu watatembelea viatu vya njumu mahali Malaika wanaogopa kukanyaga."

166 Mtawala huyu kijana kwa kweli alifanya hilo. Unaona? Alifanya ko—kosa baya mno, na tunaona kwamba halikuzuia biashara yake. Alipanuka. Alikuwa maarufu zaidi, akapata mali zaidi. Tunaona, baada ya kitambo, kwamba alikuwa mashuhuri sana mpaka hata ilimbidi kujenga maghala mapya ya kuweka chakula chake.

167 Na kwa sababu kwamba kanisa limemkataa Roho Mtakatifu, katika siku hizi za mwisho, limeongezeka. Na sasa mnaenda katika Baraza la Ekumeni, kile tu hasa Biblia ilichosema mngefanya. Sasa nyinyi ni Laodikia kweli, "tajiri na kuongezeka katika mali," kama vile tu yule kijana alivyokuwa.

168 Alikuwa mfano wa kanisa, linalokataa. Paulo alikuwa mfano wa yule anayepokea. Wote wawili walikuwa na fursa, kama ulivyo nayo usiku wa leo, nami nilivyo nayo.

169 Mali yake iliongezeka. Vivyo hivyo na kanisa, Wakati wa Laodikia, limetajirika. Pia kumbuka, alikuwa mashuhuri sana,

mpaka akapendwa sana na watu, mpaka hata watawala, watu mashuhuri, wakaanza kuja. Naye aliandaa dhifa kubwa, wakati mmoja.

170 Basi kulikuwa na mmiliki wa hati ya Uzima wa Milele kwenye duka lake kubwa, na tunaona kwamba alikuwa amelala chini kwenye mlango. Loo, huenda akafagia makombo kiasi na kumsukumia. Alikuwa na fursa tena, shahidi, Lazaro akimshuhudia. Bali yeye alifagilia tu mbali makombo, “Loo, vema, nitajaribu hii, nichukue hii robo, ama chochote,” mwajua. Hiyo karibu ndiyo nia ya 1964. “Loo, nitasaidia kidogo. Hiyo ni sawa, mwache tu aende, unaona.”

171 Lakini alishikilia hati ya mkataba. “Walio maskini katika roho,” Mathayo 5 inatuambia kwamba hao ndio, “Ufalme wa Mbingu ni wao.”

172 Aliendelea kutajirika, na kuwa mashuhuri zaidi na maarufu zaidi, na mtu mashuhuri, lakini malipo yake hatimaye yakawadia. Yalifika hatimaye. Duniani alikuwa na malipo makubwa. Alikuwa na ibada kubwa ya mazishi, bila shaka. Mhubiri mashuhuri wa kimadhehebu alikuja, labda akanena maneno makubwa juu yake. Labda walipandisha bendera nusu mlingoti. Wafanyabiashara mashuhuri walimbeba ili kumzika. Lakini Biblia ilisema, “kule kuzimu,” malipo yake yaliwadia kwa kuikataa hati ya Uzima wa Milele.

173 “Kule kuzimu aliyainua macho yake, alipokuwa katika mateso.” Basi akaangalia ng’ambo ya shimo kubwa, ambalo Yesu alisema hakuna mtu aliyewahi kulivuka ama atakayewahi kulivuka, ndipo alimpata mmiliki wa hati ya Uzima wa Milele, amefarijika, upande ule mwingine. Wote wawili. Mmoja alikuwa amepokea Hiyo. Wote wawili walikuwa na malipo yao. Mfagia makombo alipata malipo. Na sasa tajiri anakuwa ombaomba, “Mwache mmiliki wa hati ya mkataba arudi na kuigusa midomo yangu na ma—maji kidogo, kwani miale hii inanitesa.”

174 Usifanye kosa lilo hilo, ewe mfanyabiashara. Wewe ni binadamu apatikanaye na mauti kama tu walivyokuwa. Inakubidi kufanya uamuzi. Wekeza sasa. Ufanye kuwa hakika. “Fanyeni imara kuitwa kwenu, kuteuliwa.” Itoe moja ya hizo hati.

175 Tazama kwa da—dakika moja tu ama mbili zaidi, kama unaweza. Wakati Musa, aliyeacha, kuwa mfalme wa Misri, Farao, akihesabu kuwa bora aibu ya Kristo. Farao aliwaangalia watu hao kama kundi la wakanyaga matope, bali Musa aliwaona kama watu walio na ahadi.

Wewe unawaangaliaje, watu wa Mungu?

176 Musa alipata malipo yake. Waangalie waliobeba jeneza lake. Biblia ilisema walikuwa “Malaika.” Kwa nini? Hakuna mtu mwingine angaliweza kumpeleka mahali alipokuwa anaenda. Hao walikuwa ndio wabebaji jeneza lake.

177 Kulikuwa na Eliya kwenye wakati ambapo wanawake wote walinyoa nywele zao, kama Bibi Kennedy na hao wengine wafanyavyo leo hii. Wakapaka rangi nyuso zao, Yezebeli. Mfalme na watu wote waliufuata ulimwengu; kanisa lilifanya hivyo, pia. Ndipo Mungu akamtuma nabii, jina lake Eliya, kukemea kitu hicho. Baada ya yeye kuzeeka na kuchoka, alikuwa tayari kwenda Nyumbani, hata haikumbidi kufa. Malipo yake yakafika, pia, Mungu alimtumia tu gari na farasi, na kumbeba kwa hilo kwenda juu Mbinguni.

178 Stefano, aliyesimama kwenye Sanhedrin, akawanenea na kusema, "Loo, enyi wenye shingo ngumu, msiotahiriwa moyoni na masikioni, mnaoikataa hati ya mkataba, daima mnamkataa Roho Mtakatifu. Kama baba zenu walivyofanya, ndivyo mnavyofanya nyinyi." Kwenye kifo chake, alikuwa na malipo. Alitazama juu na kuona Mbingu zikifunguka, Yesu amesimama upande wa kuume.

179 Moody, siku za mwisho, yapata miaka mia moja iliyopita, maskini mshona viatu huko Chicago, hangeweza hata kuandika jina lake. Gazeti lilituma mtu kumhoji Moody, wakati mmoja. Huduma yake ilikuwa inavutia sana, walitaka kumwona waweke kwenye gazeti kilichofanya hayo; kilichomhusu Moody, kwamba alikuwa ni mhubiri wa namna gani bila shaka, na mhubiri mwenye nguvu. Kwa hiyo waliagiza mahojiano, kuandika katika maelezo yao ya mhariri. Naye Moody asingeweza hata kuyasoma hayo baada ya wao kuyaandika, kwa hiyo meneja wake ilimbidi kuyasoma kwa ajili yake. Ndipo akasema . . .

180 Hivi ndivyo maelezo hayo ya mhariri yalivyosema. Yalisema, "Kwa nini mtu yeyote aende kumsikiliza Dwight Moody akihubiri, ni zaidi ya yale niwezayo kusema." Kasema, "Kitu cha kwanza, ndiye mtu mwenye sura mbaya kuliko wote niliowahi kuona, mwenye upara na masharafa yamening'inia chini." Tena kasema, "Yeye ni—yeye ni mnene sawa na alivyo mrefu." Pia kasema, "Akijaribu kuhubiri, hawezi kusoma. Naye hutoa sauti kama mlio wa farasi anapohubiri, anazungumza kupitia pua yake, na anapiga kithembe."

181 Alipomaliza, Bw. Moody aliinua tu mabega yake, na kusema, "Hakika sivyo. Wao huja kumwona Kristo." Basi jambo lilikuwa hilo. Haijalishi kile wakosoaji walikuwa, yeye alishikilia hati ya mkataba.

182 Basi wakati alipokuwa akifa, naye daktari akasema, "Hicho ni kifo kilichopiga, Bw. Moody."

183 Alisimama, akasema, "Unakiita hiki kifo? Hii ni siku yangu ya kutawazwa." Unaona? Alishikilia ile hati ya mkataba.

184 Rafiki yangu msiri, Paul Rader. Nilipokuwa mvulana mdogo, nili—niliwekwa wakfu katika kanisa la Baptisti ya Kimishenari, naye Paul Rader alikuwa Mbaptisti ya Kimishenari pia, kwa

hiyo, Fort Wayne, nilipokuwa nimezoea kwenda kumsikia akihubiri. Baadaye, akaja hapa kwenye Pwani ya Magharibi na kupata shida nyingi sana, na hatimaye ni shida mpaka akawa mgonjwa, mwishowe ikasababisha kansa, na alikuwa yuafa. Yeye na Luke walikuwa wametembea pamoja maisha yao yote, wakashikana pamoja kama mimi na mwanangu.

185 Kwa hiyo wakati Paul alipokuwa yuafa, Taasisi ya Biblia ya Moody iliwatuma huko chini kundi la waimbaji wanne, nao walikuwa wamesimama hapo. Paul alikuwa mcheshi. Na alikuwa . . . Maskini mwenye nguvu . . . maskini Taasisi ya Biblia ya Moody, pamoja na kwaya hii, waliyokuwa wametuma huko chini, ama kundi la waimbaji wanne, nao walikuwa wanaimba, *"Karibu, Na Wewe, Mungu Wangu."*

186 Paul aligeuka na kuitupa shuka kutoka kwake. Akasema, "Ni nani anayekufa, mimi ama wewe?" Mnaona? Akasema, "Inueni hayo mapazia, na mniimbie nyimbo nzuri za Injili zinazochangamsha." Ndipo wakaanza kuimba:

> Huko chini kwenye msalaba alipofia Mwokozi wangu,
> Huko chini nililia nitakaswe kutokana na dhambi;
> Hapo ndipo Damu ilipotiwa moyoni mwangu;
> Utukufu kwa Jina Lake!

187 Paul alisema, "Yu wapi ndugu yangu, Luke?" Luke alikuwa katika chumba kingine. Hakutaka kumwona ndugu yake akifa. Kasema, "Mwambieni aje hapa."

188 Kwa hiyo Luke akaingia. Wengi wenu mlimjua, jamaa mkubwa mnene. Akaingia. Paul akanyosha mkono wake, akiwa amelala kitandani, akamshika Luke mkono na kumtazama usoni, kasema, "Luke, tumekuja kutoka mbali pamoja. Lakini wazia hili, Luke; katika dakika tano kuanzia sasa nitakuwa ninasimama katika Uwepo wa Yesu Kristo, nimevikwa haki Yake." Akishika mikono ya ndugu yake, hati yake ilimpa faida.

189 Mzee Daktari Bosworth, aliyekuwa hapa mara ya mwisho, pamoja nami, karibu mara ya mwisho, mwenye umri wa miaka themanini na nne, tukiwa ndio kwanza turudi kutoka Afrika. Nilipata wito "njoo Miami." Karibu, nipasue tairi za motokaa yangu, kufika huko. Kasema, "Alikuwa yuafa." Nikamwendea haraka. Nilijua alikuwa ni mmiliki wa hati ya mkataba. Nikaenda huko chini.

190 Nikaingia chumbani mle. Maskini jamaa huyo mwenye upara akiwa ameinua mikono yake, mikono yake midogo iliyokonda. Nikamkimbilia na kuinamisha uso wangu, na kulia, "Baba yangu, baba yangu, gari la Israeli na wapanda farasi wake!" Akaweka mikono yake juu yangu na kunibariki.

Nikasema, "Ndugu Bosworth, ninaweza kukuombea?"

Kasema, "La." Kasema, "Mimi si mgonjwa."

Nikasema, "Kuna nini, Ndugu Bosworth?"

Kasema, "Ninaenda tu Nyumbani."

191 Nikasema, "Nilijua hilo." Ndipo nikasema, "Ninataka kukuuliza jambo fulani, Ndugu Bosworth." Nikasema, "Ni wakati gani uliokuwa mkuu kuliko zote za maisha yako na huduma yako? Ulikuwa ukimtumikia Mungu kabla sijazaliwa. Tumekuwa katika huduma za umishenari pamoja. Tumekuwa katika dhoruba, angani na baharini. Ulisimama nami wakati nilipoona ibilisi katika kila upande, na wachawi. Na kulikuwa na misisimko mikubwa tulipomwona Mungu akiwaduwaza huku tumesimama pale. Msisimko mkubwa kuliko yote ya maisha yako ulikuwa upi?"

192 Akasema, "Sasa hivi." Alikuwa anajitayarisha kupokea malipo ya hati yake ya mkataba. Akasema, "Yote niliyoishia, Ndugu Branham, yamekuwa ni Yesu Kristo, na dakika yoyote Yeye ataingia mlangoni kunipeleka Nyumbani."

193 Naam, hao walikuwa ni wamiliki wa hati waliotoa kila kitu walichokuwa nacho, na kuwekeza katika Lulu yenye thamani kubwa. Hivi hutawekeza, usiku wa leo, pia, huku tukiinamisha vichwa vyetu?

194 Siwezi kuona kupita wasikilizaji. Sijui kilicho. . .ni wangapi, ama ni nani anayetazama, kwenye televisheni ya nyaya maalum usiku wa leo. Ninaenda kukuuliza, ewe rafiki, hebu haya yasiwe maneno ya bure. Wewe ni mwanadamu. Huna budi kufa. Unajua hilo. Na huenda ikawa ni kabla ya asubuhi wakati wako utakapowadia. Mimi si. . .mtu anayependa sana kushawishi; na, kwa sababu Yesu alisema, "Wote alionipa Baba watakuja." Kama kuna nafasi moyoni kwa ajili ya hati hiyo, usiku wa leo, hivi hutaikubali Hiyo? Hati hiyo ni Kristo, hati ya toleo la upendo wa Mungu kwako, Neno Lake kuwa hai ndani ya moyo wako, kukufanya wewe sehemu Yake. Yeye ni Neno. Mkubali Yeye maishani mwako. Je! hutafanya hivyo, na kufanya uwekezaji huu mkuu?

195 Kadri ninavyoweza kuona, siwezi kuona ila tu yapata futi kumi kutoka mahali nilipo, ama kumi na tano. Ninaenda kuwaombeni mwinue mikono yenu kama mngetaka kupokea moja ya hati za Uzima wa Milele. Useme, "Ninaitaka, Ndugu Branham. Nikumbuke tu katika maombi yako. Huuoni mkono wangu, bali Mungu anauona."

196 Baba yetu wa Mbinguni, hadithi hii ya maisha rahisi, fidhuli, na hata hivyo ni kweli. Niliinena kwa njia hii, Bwana, kwa sababu kwamba watu, watu wafanyabiashara, wangeielewa zaidi katika njia ya kitu kuwakilishwa hapa duniani. Hiyo ndiyo sababu ninaiita hati ya mkataba. Nisamehe kama nilikosea kwa kuiita hivyo. Kwa kuwa, sasa tuko katika wa—wakati wa kicho sana, ambapo hapana shaka kwamba wapo wengi wanaowazia

kwa makini sasa, wakijua kwamba wao pia itawabidi kuwa na malipo juu ya chochote walicho nacho hapa, nao wanaona kinachomaanisha kukataa.

197 Sasa, yule kijana, kama nijuavyo, labda akiwa maarufu sana miongoni mwa watu, alibaki kanisani, alitii amri, hakufanya uzinzi, wala kuiba, au kufanya mambo hayo, bali katika moyo wake mwenyewe alijua kwamba hakuwa na Uzima wa Milele. Wafanye hao, Bwana, ambao wanajaribu kukutana na Wewe, kwa ajili ya Uzima wa Milele, wakiwa tu na hizo sifa za uadilifu, jalia usiku wa leo wapokee mwaliko, na kukaa tu miguuni mwao, na kusema, "Bwana, nitafanya lolote Wewe utakalonitaka nifanye." Tujalie, Bwana.

198 Wote ni Wako sasa. Ninakabidhi kila kitu Kwako. Na ikiwa mbegu imeanguka mahali popote, Bwana, mahali popote, mbegu yoyote teule, kwa miaka mingi imekuwa ikiona njaa na kiu, huenda imewaangukia wengine mahali fulani usiku wa leo. Jalia wapokee Uzima, Baba, kwa kuwa ninaomba hayo katika Jina la Yesu Kristo.

199 Na huku tukiendelea kuviinamisha vichwa vyetu, nitamwomba Ndugu Pearry, kama ataweza, aje hapa na aendelee, achukue sehemu iliyobaki ya ibada.

Uwekezaji SWA64-0314
(The Investments)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumamosi jioni, tarehe 14 Machi, 1964, kwa ajili ya dhifa ya Shukrani ya Wafanyabiashara katika Hoteli ya Beaumont kule Beaumont, Texas, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2019 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org